**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA**

# TAARIFA FUPI YA MIRADI ITAKAYOPITIWA NA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2024

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2024;*** Mwenge wa Uhuru utakimbizwa kwa kilomita **221.7** katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na utapita katika miradi **07** inayolenga sekta za uchumi na huduma za jamii yenye jumla ya gharama ya **Tsh.1,284,109,427.50** Kati ya hizo Tsh **1,069,991,727.50 ni** Fedha za Serikali Kuu, **Tsh 154,662,000.00** ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri Tsh **45,328,100.00** ni nguvu za wananchi, Tsh **9,230,000.00** ni fedha za michango ya Mwenge Tsh **1,440,000.00** ni fedha za Mfuko wa jimbo na Tsh **3,457,600.00** ni fedha za Wadau wengine wa Maendeleo.

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru;*** Mwaka 2024 Mwenge wa Uhuru unategemewa kufungua Miradi 2, Ujenzi wa Madarasa 4 na Matundu 4 ya vyoo shule ya Sekondari Songwe wenye thamani ya Tsh **114,477,200.00**, na Mradi wa Maji Simambwe wenye thamani ya Tsh **655,889,027.5** Miradi itakayowekewa jiwe la msingi ni miradi 2 ambayo ni Jengo la upasuaji kituo cha afya Igoma wenye thamani ya Tsh**145,910,500.00** na Mradi ujenzi wa daraja la Imezu wenye thamani ya Tsh **118,531440.00**.

Miradi 2 itatembelewa na kukaguliwa ambayo ni mradi wa uhifadhi wa Msitu wa Ikhoho unaogharimu Tsh **9,450,000** kila mwaka kwa ajili ya utunzaji wake na Mradi wa Kikundi cha Vijana Gombe wanaojihusisha na usafirishaji Abiria (Bodaboda) wenye thamani ya Tsh **49,500,000.00.**

Watoto wanaopata Fursa za Elimu wenye Mahitaji Maalumu ambapo Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya inachangia kiasi cha Tsh **186,123,672.00** kwa ajili ya chakula kwa mwaka watatembelewa na kugaiwa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Tsh **4,230,000.00** shule ya Msingi Nsalala (Ndola/Muungano)

## TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOPITIWA NA MWENGE WA UHURU HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA

| NA | JINA LA MRADI | IDARA/KIGEZO | ENEO | SHUGHULI | SERIKAL KUU | HALMASHAURI | N/WANANCHI | W/ WA MAENDELEO | M/ YA MWENGE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa jengo la upasuaji kituo cha afya Igoma | AFYA | INYALA | JIWE LA MSINGI | - | 110,000,000 | 34,470,500 | 1,440,000 | | 145,910,500 |
| 2 | Mradi wa Maji wa Simambwe | MAJI | TEMBELA | UZINDUZI | 655,889,027.50 | | | | | 655,889,027.50 |
| 3 | Uhifadhi wa Msitu wa Ikhoho | MALIASILI | TEMBELA | KUKAGUA | 9,450,000 | | | | | 9,450,000 |
| 4 | Ujenzi wa Daraja la Imezu | BARABARA/DARAJA | INYALA | JIWE LA MSINGI | 118,531,440 | | | | | 118,531,440 |
| 5 | Mradi wa fursa za Elimu kwa watoto wenye mahitaji maalumu | MAHITAJI MAALUMU | NSALALA(Ndola/Muungano) | KUKABIDHI VIFAA | 186,121,260 | | | | 4,230,000 | 190,351,260 |
| 6 | Kikundi cha Vijana Gombe, Usafirishaji abiria (Bodaboda) | UWEZESHAJI WA VIJANA | B/SONGWE | KUTEMBELEA | - | 40,500,000 | 9,000,000 | | | 49,500,000 |
| 7 | Ujenzi wa Vyumba 4 vya madarasa na Matundu 4 ya vyoo shule ya Sekondari Songwe | ELIMU | B/SONGWE | UZINDUZI | 100,000,000 | 4,162,000 | 1,857,600 | 3,457,600 | 5,000,000 | 114,477,200 |
| | JUMLA | | | | **1,069,991,727.50** | **154,662,000** | **45,328,100** | **4,897,600** | **9,230,000** | **1,284,109,427.50** |

## NJIA NA MATUKIO YA MWENGE WA UHURU KWA MWAKA 2024

| MUDA | MAHALI | UMBALI | TUKIO | MHUSIKA |
|---|---|---|---|---|
| *12:00Asb - 1: 00Asb* | *Kijiji cha Simambwe* | *0* | *Mapokezi ya Mwenge wa Uhuru toka Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo* | ***DC*** |
| | | | *Utambulisho* | ***DC*** |
| | | | *Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| | | | ***CHAI*** | |
| *1:30 Asb - 2:30 Asb* | *IGOMA* | *25* | *Uwekaji wa jiwe la Msingi Ujenzi wa Jengo la Upasuaji Kituo cha afya tarajiwa Igoma* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| *2:30 Asb - 3:00 Asb* | *SIMAMBWE* | *25* | *Uzinduzi wa Mradi wa Maji* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| *3:00 Asb - 4:00 Asb* | *TEMBELA* | *5* | *Kukagua Mradi Uhifadhi wa Msitu wa Ikhoho* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| *4:00 Asb - 5:30 Asbh* | *INYALA* | *16.7* | *Kuweka jiwe la Msingi Daraja la Imezu* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| *6:30 Asb - 7:00 Mch* | *NSALALA (MUUNGANO S/M)* | *40* | *Kugawa mahitaji kwa watoto wenye mahitaji maalumu Shule ya Msingi Muungano, Uzinduzi Klabu ya Rushwa na kuona uendelevu wa mradi wa daraja la Nsenga uliozunduliwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2023* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| *7:00 Mch - 8:00 Mch* | *MUUNGANO SM* | *0* | ***CHAKULA CHA MCHANA*** | ***DC*** |
| *8:00Mch - 8:30Mchn* | *BONDE LA SONGWE* | *5* | *Kutembelea Mradi wa Kikundi cha Vijana Maafisa Usafirishaji Gombe Ifisi* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| *8:30Mch - 9:30Mch* | *BONDE LA SONGWE* | *15* | *Uzinduzi wa Madarasa 4 na matundu 4 ya Vyoo Songwe Sekondari* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| *9:30Mch - 11: Jioni* | *UTENGULE USONGWE* | *20* | ***ENEO LA MKESHA*** *Kongamano la Vijana, Ukaguzi wa mabanda, Usomaji wa risala ya Utii, Ujumbe wa Mwenge* | *Kiongozi wa Mbio za Mwenge* |
| *11:00 Alf - 1:00 Asbh* | *SONGWE* | *70* | ***MAKABIDHIANO IFWENKENYA*** | ***RC*** |
| | | *221.7* | | |

**TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA JENGO LA UPASUAJI KITUO CHA AFYA TARAJIWA IGOMA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2024, NDG. GODFREY ELIAKIMU MNZAVA LEO TAREHE 30/08/2024.**



***Mwonekano wa Jengo la Upasuaji kituo cha Afya Tarajiwa Igoma katika picha***

## 1.0 UTANGULIZI.

**Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024;**

Mradi huu wa Ujenzi wa Jengo la Upasuaji katika kituo hiki cha afya tarajiwa Igoma ulianza tarehe 15/02/2020 kwa Nguvu za Wananchi kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na wadau mbali mbali wa Maendeleo. Wananchi wa vijiji vya Kimondo, Igoma na Mwanzazi, wapatao Elfu sita mia moja sabini na mbili (6,172) katika kata ya Igoma walihamasika na kuona umuhimu wa kusogeza huduma ya Afya karibu yao, hivyo walianza kwa kuunda kamati za ujenzi, kuhamasishana kusogeza fursa kama mawe mchanga, tofali, kuchota maji, usafishaji wa eneo, kujenga msingi na kupandisha boma la jengo la upasuaji na kuliezeka kwa nguvu zao wenyewe, Michango hii ya nguvu kazi za wananchi inakadiriwa kuwa na thamani ya Tsh 34,470,500.00. Halmashauri katika kutambua jitihada hizi za wananchi ilitoa fedha kiasi cha Tsh 110,000,000 katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la Upasuaji kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri.

## 2.0 GHARAMA ZA MRADI NA MAPOKEZI FEDHA

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024,*** Mradi huu wa kituo cha Jengo la Upasuaji katika kituo cha afya tarajiwa Igoma unategemea kugharimu kiasi cha Tsh 150,211,905.00 hadi kukamilika kwake, Mradi huu unatekezwa kwa Mapato ya ndani, Nguvu za wananchi na wadau wa maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Agosti 2024, Jumla ya **Tsh 145,910,500.00** zimepokelewa kutoka Mapato ya ndani ya Halmashauri, Michango ya wananchi, Mfuko wa Jimbo na wadau wengine wa maendeleo.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MRADI NA MATUMIZI YA FEDHA

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024*;** Mradi huu unatekelezwa kwa njia ya force account. Mradi upo kwenye hatua za ukamilishaji kwa asilimia (95) kazi ambazo hazijafanyika ni umaliziaji wa chumba cha upasuaji kwa kuweka sakafu maalum na kuweka sinki pamoja na ununuzi wa vifaa vya upasuaji

Aidha hadi kufikia Mwezi Agosti 2024, kiasi cha Tsh **103,898,100.00** kimetumika ikijumuisha kiasi cha Tsh **34,470,500.00** thamani ya nguvu na michango ya wananchi na wadau wengine wa maendeleo na kubakiwa na Tsh **42,012,400.00** Fedha zilizotumika zimetumika kununua vifaa vyote vya ujenzi na kulipa mafundi. Fedha zilizobaki ni kwa ajili ya kulipa mafundi watakapomaliza kazi zilizobaki za kuweka sakafu maalumu ya chumba cha upasuaji (Epoxy) pamoja na kununua Masinki (scrub na sluice sink), na ununuzi wa samani. Jedwali lifuatalo linaonyesha kwa mchanganuo mapokezi na matumizi ya fedha hizi.

| NA. | CHANZO CHA FEDHA | KIASI KILICHOTOLEWA | KIASI KILICHOTUMIKA | BAKAA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Michango ya nguvu za wananchi* (fursa zilizothamanishwa) | 34,470,500.00 | 34,470,500.00 | - |
| 2. | Mapato ya ndani ya Halmashauri | 110,000,000.00 | 67,987,600.00 | 42,012,400.00 |
| 3. | Mfuko wa Jimbo | 1,440,000.00 | 1,440,000.00 | - |
| | **Jumla** | **145,910,500.00** | **103,898,100.00** | **42,012,400.00** |

## 3.0 MANUFAA YA MRADI.

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024*;** Mradi huu utakapokamika utakuwa na manufaa yafuatayo.

- Utasogeza huduma ya Afya bora zaidi kwa wananchi hasa ukizingatia wananchi wanaifuata huduma hii Hospitali ya Jiji Igawilo iliyopo kata ya Iganjo Mtaa wa Ikanga umbali wa km 30 kutokea kata ya Igoma
- Wajawazito watakaotakiwa kupata huduma ya upasuaji wataipata huduma hii katika kituo cha Afya Igoma.
- Kutapunguza wimbi kubwa la wajawazito kujifungulia majumbani chini ya wakunga wa jadi, mazingira ambayo hupelekea vifo vya watoto wachanga na kina Mama.

## 5.0 HITIMISHO.

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024*;** tunapenda kuchukua fursa hii kuishukuru serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kimaendeleo hususani katika sekta ya Afya. Ikiwa ni utekelezaji wa ILANI ya uchaguzi wa chama cha mapinduzi (CCM) ya mwaka2020-2025 ibara ya 83(d) kujenga na kuimarisha vituo vya kutolea huduma za Afya ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi.

***Ndugu kiongozi wa mbio za mwenge wa uhuru kitaifa 2024***, Kwa heshima kubwa tunakuomba sasa utuweke jiwe la msingi katika mradi huu wa ujenzi wa jengo la upasuaji kituo cha afya tarajiwa Igoma

Sisi Wananchi wa Kata ya Igoma tunaungana na KAULI MBIU iseamayo

***"Tunza Mazingira, na shiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ujenzi wa Taifa endelevu"***

**DR AHMADI SELEMANI**
**KNY; MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA MBEYA**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA MAJI SIMAMBWE KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA 2024, NDG. GODFREY ELIAKIMU MNZAVA LEO TAREHE 30/08/2024




***Mwonekano wa Tank la kuhifadhia maji Mradi wa Maji Simambwe katika picha***

## 1.0 UTANGULIZI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Wakala wa maji na usafi wa mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mbeya kwa Kushirikiana na RUWASA Mkoa wa Mbeya imetekeleza ujenzi wa mradi wa maji katika vijiji vya Simambwe, Shibolya, Ilembo Usafwa na Usoha Njiapanda Kata ya Tembela, Mradi huu umetekelezwa kwa kutumia mkandarasi EA BUILDERS LTD. Ujenzi wake ulianza kutekelezwa tarehe 15/05/2022 na kukamilika tarehe 30/01/2024, Mradi huu unatumia chanzo cha Chem chem ya **Salalani** chenye uwezo wa lita **10.1** kwa sekunde, kilichopo katika eneo la kijiji cha Simambwe kata ya Tembela.

## 2.0 LENGO LA MRADI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Lengo la mradi huu ni kuwapatiwa huduma ya maji safi na salama wakazi wapatao 6,974 wa Vijiji vya Simambwe, Shibolya, Ilembo Usafwa na Usoha Njiapanda kwa kutekeleza shughuli zifuatazo; Ujenzi wa banio la maji, ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ukubwa wa mita za ujazo 250 (Lita 250,000), ujenzi wa tanki dogo la kuhifadhia maji (Sump wells) mita za ujazo 30 (Lita 30,000), ujenzi wa nyumba ya mitambo, ujenzi wa vituo 31 vya

kuchotea maji, unganishaji wa umeme wa grid ya taifa, ufungaji wa pampu ya umeme (submersible pump) na ulazaji wa mtandao wa bomba wenye urefu wa mita 17,345.

### 3.0 GHARAMA ZA UTEKELEZAJI WA MRADI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Mradi huu umetekelezwa kwa fedha za Serikali kupitia Mfuko wa Maji wa Taifa, ambapo makadirio ya mradi huu yalikuwa ni Tsh **636,703,228.88** na thamani ya kazi zilizofanyika ni **Tsh 655,889,027.50** hadi sasa tumepokea kiasi cha Tsh **488,913,979.00**, na fedha yote amelipwa mkandarasi.

### 4.0 MAFANIKIO

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Mafanikio ya mradi huu una uwezo wa kuhudumia wakazi wapatao 6,974 wa Vijiji vya Simambwe, Shibolya, Ilembo Usafwa na Usoha njiapanda na pia umetoa ajira kwa wananchi 53, (Wanaume ni arobaini na nne (44) na Wanawake ni tisa (9).) Sambamba na kuondokana na maradhi ya matumbo ya kuhara na pamoja na kuboresha vipato vyao kwani muda mwingi ulitumika kusafiri umbali mrefu kwenda kutafuta huduma ya maji. Ili mradi uweze kuwa endelevu tayari tumeunda chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya Jamii (CBWSOs) ili kuweza kusimamia utoaji wa huduma ya maji.

### 5.0 HITIMISHO

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha huduma ya maji katika Wilaya yetu kwa kutoa fedha za ujenzi wa Miradi ya Maji.

Ndugu Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, kwa heshima na tahadhima sasa nakuomba uipokee taarifa hii, ukague na kuzindua mradi huu.

***"Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu"***

MHANDISI; SAMBWE P. SIJABAJE

**MENEJA RUWASA.**

**WILAYA YA MBEYA**

# TAARIFA YA MSITU WA HIFADHI WA IKHOHO KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2024; NDG. GODFREY ELIAKIMU MNZAVA LEO TAREHE 30.08.2024



***Mwonekano wa Msitu wa hifadhi Ikhoho katika Picha***

## 1.0. UTANGULIZI.

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Msitu wa hifadhi Ikhoho ni msitu wa Serikali kuu unaosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii. Msitu huu ulihifadhiwa kisheria mwaka 1935 kwa tangazo la serikali namba 126 na una ukubwa wa Hekta 1,416.

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,***
Msitu wa hifadhi Ikhoho upo umbali wa kilometa 25 Mashariki mwa jiji la Mbeya, msitu huu umepakana na kata mbili za Maendeleo na Tembela. Kata ya Maendeleo ina vijiji 3 vya Usohamuungano, Izumbweusafwa na Ikhoho na kata ya Tembela ina vijiji 3 vya Usohanjiapanda, Ilembousafwa na Shibolya.

## 2.0. UMUHIMU WA MSITU WA HIFADHI IKHOHO.

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024***, Umuhimu wa hifadhi ya Msitu wa Ikhoho umeainishwa kama ifuatavyo**;**

- Utunzaji wa vyanzo vya maji – msitu huu una mito miwili (2) mikubwa ya Mlowo na Patagwa ambayo hupeleka maji yake mto Ruaha Mkuu na hatimaye maji yake kutiririka mpaka bwawa la Mwl. Nyerere.
- Utunzaji wa bioanuai iliyopo (wanyama na mimea)-Msitu wa hifadhi Ikhoho una mimea na miti ya aina mbalimbali ambayo ipo hatarini kutoweka kama haitatunza vizuri, aidha kuna wanyama wadogo kama nyani, nyoka, ndege na wadudu wa aina mbalimbali; hivyo msitu huu ni makazi ya Wanyama na viumbe hai wengine.
- Hifadhi ya mazingira na utunzaji wa ardhi kwa ujumla.
- Msitu huu hurekebisha hali ya hewa na kupambana na mabadiliko ya tabia nchi.

- Msitu huu hutumika kwa matambiko ya kimila pamoja na dawa za asili.

## 3.0 MIKAKATI YA UTUNZAJI WA MSITU.

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024***, Mkakati ya utunzaji wa Msitu ni kama ifuatavyo;

- Kutoa elimu ya utunzaji mazingira kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya pamoja Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwenye vijiji vinavyozunguka Msitu kwa njia ya mikutano ya hadhara, vipindi vya redio na majarida.
- Kushirikisha viongozi wa kata/vijiji katika utunzaji wa msitu.
- Kuwashirikisha Machifu wa maeneo husika katika utunzaji wa msitu.
- Kuimarisha mipaka ya msitu kwa kuweka mabango na beacons.
- Doria za mara kwa mara kwa ajili ya kudhibiti uvamizi wa msitu.

## 4.0 USHIRIKISHWAJI WA JAMII KATIKA UTUNZAJI WA MSITU.

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** jamii ya vijiji vinavyozunguka Msitu wa hifadhi Ikhoho hushirikishwa katika utunzaji wa msitu kwa kufanya doria za mara kwa mara, aidha wananchi hupewa miche ya miti bure kwa ajili ya kupanda kwenye mashamba yao, katika sehemu zilizoharibika pamoja na kupanda kwenye vyanzo vya maji.

Njia nyingine ya ushirikishwaji ni kutoa vibali vya ufugaji wa nyuki kwa wananchi kwa kutundika Mizinga ya kisasa ndani ya hifadhi.

## 5.0 GHARAMA ZA UTUNZAJI MSITU.

- Gharama za utunzaji wa msitu wa hifadhi Ikhoho zikijumuisha doria pamoja na uimarishaji wa mipaka ya msitu jumla ni **Tshs 9,450,000.00** kila mwaka.
- Wananchi wanamchango katika uhifadhi wa Msitu ambapo kuna kamati za mazingira za vijiji ambazo pamoja na majukumu yao mengine hufanya doria za mara kwa mara ili kudhibiti uharibifu usitokee na kuzima moto pale unapotokea.

## 6.0 HITIMISHO

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** tunakuomba sasa utembelee na ukague msitu wa hifadhi Ikhoho, Sisi wananchi wa Ikhoho tunaungana na Kauli mbiu Isemayo;

“***Tunza mazingira na shiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu.***”

EUNICE NELSON MBILINYI
**MHIFADHI MISITU (TFS)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA.**

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI-TANZANIA (TARURA)

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY
TARURA
Improved Roads For Sustainable Development

Ofisi ya Meneja (W),
S.L.P. 2195,
**Mbeya**.

## TAARIFA YA UJENZI WA DARAJA LA IMEZU KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA, 2024 BW. GODFREY ELIAKIMU MNZAVA LEO TAREHE 30.08.2024



**Picha:** *Kabla ya Ujenzi wa Daraja*



**Picha:** *Baada ya Ujenzi wa Daraja*

## 1.0 UTANGULIZI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Daraja la IMEZU lenye urefu wa mita 7, upana wa mita 5.7 na kina cha Mita 4 katika barabara ya Imezu - Darajani Kata ya Inyara, limejengwa na mkandarasi **M/S E.A BUILDERS Limited** wa **S.L.P 897, MBEYA**. Mradi huu umetokana na umuhimu katika jamii kwa kuwa ni Daraja pekee linalounganisha Wilaya ya Mbarali. Ujenzi wa Daraja hili ulianza tarehe 18/09/2023 na utakamilika tarehe 20/06/2024.

## 2.0 GHARAMA ZA MRADI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Ujenzi wa daraja la Imezu unagharamiwa na fedha za Matengenezo ya barabara kiasi cha TZS. **118,531,440.00** (Milioni Mia moja kumi na nane, mia tano thelathini na moja elfu na mia nne arobaini). Hadi sasa fedha iliyolipwa kwa Mkandarasi ni kiasi cha TZS. **82,420,040.00** sawa na **69.5%** ya Mkataba wake. Kiasi cha fedha kilichoshikiliwa (Retention Money) kwa mujibu wa mkataba ambacho kitalipwa baada ya muda wa

matazamio kuisha (Defect Liability Period) ni TZS. **8,242,004.00** ambayo itafanya jumla ya **TZS. 95,647,720.00** sawa na **(80.69%)** ya kazi zote alizofanya.

## 3.0 MANUFAA YA MRADI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Mradi huu unafaida mbalimbali kama ifuatavyo: -

1. Kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji wa haraka kwa wananchi wanaohitaji huduma za kijamii katika kata ya Inyala.
2. Kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji wa haraka wa mazao kutoka kata ya Inyala na nje ya kata hiyo kwenda kwenye eneo la Soko.
3. Kuchochea shughuli za kiuchumi, ajira na kipato kwa Wananchi wa kata za Inyala na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Mbarali kwa ujumla.
4. Kutoa ajira za muda mfupi ambapo jumla ya watu 30 waliajiriwa kama vibarua wa muda kati ya hao wanawake walikuwa 8 na wanaume 22

## 4.HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Ujenzi wa daraja la Imezu umekamilika kwa **80.69%**. Ujenzi wa mradi huu umetumia Mfumo wa **Kandarasi**. Wananchi wameshirikishwa kikamilifu tangu mradi unaanza hadi kufikia hatua iliyopo sasa. Wakati wa utekelezaji wa Mradi hapakuwa na changamoto yoyote iliyojitokeza ambayo ingekwamisha mradi kutofanyika.

## 5.0 HITIMISHO

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024,*** Tunatoa shukrani kwa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizotumika kugharamia ujenzi wa mradi huu kama Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 inavyoelekeza katika Ibara ya 56 (a). Pia tunatoa shukrani kwako Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa kwa kukubali kuja kuungana nasi kuweka jiwe la Msingi katika daraja la Imezu.

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa 2024*** Kwa heshima na taadhima, tunakuomba sasa utuwekee jiwe la Msingi katika Mradi wa Ujenzi wa daraja la Imezu. Sisi wananchi wa Inyala tunaungana na Kauli mbiu Isemayo;

"***Tunza mazingira na shiriki uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu."***

Mhandisi; BONIFACE KASAMBO
**MENEJA WA TARURA.**
**WILAYA YA MBEYA**




***Mwonekano wa baadhi ya vifaa vya Watoto wenye Mahitaji Maalum katika Picha***

## 1.0 UTANGULIZI.

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024;*** Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya inatoa huduma na fursa za kielimu kwa makundi maalum ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu wenye Ulemavu wa akili, Ulemavu wa viungo, albino, viziwi na wasioona na kufanya kuwa na jumla ya wanafunzi 585, wakiwemo Wavulana 331 na Wasichana 254.

## 2.0 LENGO LA UTOAJI WA FURSA HIZI

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024;*** Lengo la Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ni kuwapa fursa za Kielimu wanafunzi wenye mahitaji maalum na huduma nyingine za kijamii.

## 3.0 GHARAMA ZA MRADI.

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024;*** Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya inatoa jumla ya **Tshs 186,121,260.00** kila mwaka kwa ajili ya chakula cha Watoto wenye mahitaji maalum ikiwa ni Tshs **318,156.00** kwa kila mwanafunzi mwenye mahitaji maalum kwa wanafunzi **585**. Aidha kiasi cha Tsh **4,230,000.00** kimetolewa kwenye fedha za Mchango wa mwenge kwa ajili ya kununua

vifaa saidizi na vifaa vya kufundishia vikiwemo Viti mwendo, Mafuta ya kuzuia jua na kofia kwa ajili ya Watoto wenye ulemavu wa Ngozi, midoli, na shimesikio.

## 4.0 MANUFAA YA FURSA ZA KIELIMU

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024*;** huduma zinazotolewa ni pamoja na manufaa ya kielimu na kijamii kama kujipatia ajira. Mipango mikakati ya utoaji fursa hii kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ni kuendelea kuhudumia kundi hili, kuendelea kubaini watoto wenye ulemavu wanaofichwa nyumbani na kuwashirikisha kwenye michezo ngazi ya shule hadi Kitaifa.

## *5.0 HITIMISHO*

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024*;** Naomba kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mh. Dkt.Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuboresha Elimu na kuwajali Watoto wenye Mahitaji Maalum nchini. Kwa heshima kubwa tunakuomba Ukabidhi vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum hapa Shule ya Msingi Muungano kwa wawakilishi wa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

KAULI MBIU ***"Tunza Mazingira, na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu".***

***Mwenge wa Uhuru Kitaifa Hoyeeeeeeeeeeee***

**TANU KAMEKA**
**KNY; MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**MBEYA.**

**TAARIFA YA KLABU YA WAPINGA RUSHWA SHULE YA MSINGI MUUNGANO ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDUGU GODFREY ELIAKIMU MNZAVA TAREHE 30/08/2024**

## 1.0 Utangulizi

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024***, tunayo furaha kubwa kukukaribisha wewe binafsi pamoja na msafara wako katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, katika shule yetu ya Msingi Muungano.

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024,*** Klabu yetu ya kupambana na kudhibiti Rushwa katika Shule ya Msingi Muungano ina jumla ya wanachama 100, wavulana 50 na wasichana 50,Kama tujuavyo sote, jukumu la mapambano dhidi ya Rushwa si la TAKUKURU pekee, bali ni la Watanzania wote ili kuwa na Taifa lenye uadilifu kufikia uchumi wa viwanda.

## 2.0 MALENGO YA CLUB

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024,*** malengo ya klabu yetu ni kama yafuatayo; -

1. Kutoa Elimu dhidi ya athari za RUSHWA NA DAWA ZA KULEVYA kwa wanafunzi na jamii inayotuzunguka na Taifa kwa ujumla.
2. Kujenga maadili mema kwa watoto wakiwa na umri mdogo.
3. Kujenga uelewa wa athari za RUSHWA NA DAWA ZA KULEVYA katika jamii, hii itawafanya kufahamu namna ya kuviepuka hivyo.
4. Kujenga ujasiri wa kukataa kushiriki katika vitendo vya RUSHWA NA DAWA YA KULEVYA.

## 3.0 MAFANIKIO YA KLABU

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024,*** Klabu imefanikiwa;-

1. Kutoa semina kwa wanafunzi wenzetu juu ya athari mbalimbali za RUSHWA NA DAWA ZA KULEVYA ambazo ni hatari kwa mtu mmoja mmoja, jamii, na taifa kwa ujumla. Katika kufikisha ujumbe huu tumetumia Maigizo, majigambo, mashairi na ngonjera kuelimisha wanafunzi juu ya kuwa jasiri kwenye mapambano dhidi ya RUSHWA NA DAWA ZA KULEVYA.
2. Kutembelewa na viongozi kutoka Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Mbeya na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kanda ambapo tumekuwa tukipewa elimu, miongozo na machapisho mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uelewa.

## 4.0 HITIMISHO

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024,*** tunayo furaha kubwa kutoa shukrani zetu za dhati kwako kwa kukubali kulipokea jukumu kubwa la kuimulika nchi yetu yote na mipaka yake. Aidha, tunashukuru sana kwa ujio wako hapa shuleni kwetu kuja kuzindua KLABU YETU YA WAPINGA RUSHWA.

Pamoja na kukubali kuizindua klabu yetu ya **"WAPINGA RUSHWA".** Tunakuombea kwa Mungu akulinde na kukutunza wewe na msafara wako wote hadi hitimisho la mbio hizi za mwenge wa uhuru kitaifa za mwaka 2024.

**'KUZUIA RUSHWA NI JUKUMU LAKO NA LANGU TUTIMIZE WAJIBU WETU'.**

**"MWENGE WA UHURU OYEEEEEEEEEEEEEEEE".**

**GLORY GASPER JOHN**
**MWENYEKITI WA KLABU**
**SHULE YA MSINGI MUUNGANO**

**TAARIFA YA MRADI WA KIKUNDI USAFIRISHAJI GOMBE KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE KITAIFA MWAKA 2024, NDUGU GODFREY ELIAKIMU MNZAVA LEO TAREHE 30.08.2024.**




***Kikundi cha Vijana Gombe katika picha***

**1.0 UTANGULIZI.**

**Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru kitaifa wa Mwaka 2024**, kikundi cha Gombe ni kikundi cha Vijana (wakiume) wanaojishughulisha na usafirishaji wa abiria kwa kutumia pikipiki. Kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2019 kikiwa na wanachama 16. Kwa sasa wamebaki vijana 8 wengine 8 wamekosa sifa ya kuendelea kuwa wanakikundi kutokana na kuzidi umri hivyo wamebaki kuwa washauri. Kikundi kinapatikana Kata ya Bonde la Songwe, kijiji cha Ikumbi, kitongoji cha Ifisi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

**2.0 HISTORIA YA MRADI.**

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa* wa Mwaka 2024*,*** Kikundi hiki kilibuni mradi ili kuzalisha ajira kwa vijana ndani ya kikundi, pia kuongeza kipato cha mwanakikundi mmoja mmoja, familia na Jamii kwa ujumla. Kikundi cha vijana Gombe kilianza na mradi wa kuweka na kukopa kwa mtaji wa **Tshs. 600,000.00** kwa lengo la kujikwamua kiuchumi na kusaidiana katika shida na raha**.** Kikundi kinajishughulisha na kuweka na kukopa pamoja na usafirishaji abiria kwa kutumia pikipiki (Bodaboda) ili kujiongezea kipato.

**3.0 GHARAMA ZA MRADI.**

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024***. Mtaji wa kikundi hiki ni kiasi cha **Tshs. 49,500,000.00** kati ya fedha hizo kiasi cha **Tshs.40,500,000.00** ni mkopo kutoka Halmashauri zilizokopeshwa mwezi Machi 2022 ikiwa ni asilimia 4 katika asilimia 10 zinazochangiwa katika Mfuko wa Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu toka mapato ya ndani. Fedha hizi zilitumika kununua pikipiki 16 kwa ajili ya biashara ya usafirishaji wa abiria na Tsh **9,000,000.00** ni fedha zilizopatikana kutokana na shughuli za ukopeshanaji wa wanakikundi wenyewe ambazo tunaendelea kukopeshana. Aidha fedha zilizotolewa na Halmashauri zote zimerejeshwa kama ilivyotakiwa.

## 4.0. MAFUNZO

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa mwaka 2024,***
Kabla ya kupata mkopo huu; Halmashauri walitupa mafunzo vikundi vyote 11 vilivyokopeshwa fedha. Mafunzo hayo yalihusu ujasiriamali, Usalama barabarani, Rushwa, Utunzaji wa kumbukumbu, mipango na bajeti, Bima, utunzaji wa fedha, usimamizi wa miradi. urejeshaji wa fedha za mkopo, Uongozi, Jinsia na Ukimwi.

## 5.0 MALENGO YA KIKUNDI

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa mwaka 2024,***
Kikundi kina Malengo yafuatayo;

- Kujikwamua kiuchumi kutokana na mradi wa usafirishaji wa abiria ambapo Mikopo ya Halmashauri ilitutaka kurejesha wastani wa Tsh 7,031 kwa siku bila riba tofauti na Mikataba tuliyokuwa tunaingia na wamiliki binafsi ya Marejesho ya Tsh.10,000.00 kwa siku.
- Kujikomboa na Mikataba kandamizi isiyoangalia hali halisi ya kipato kinachoweza kupatikana kwa siku, Mikataba ambayo ilikuwa inatutaka kurejesha fedha kiasi cha Tsh 10,000.00 kila siku kwa mwenye mali.
- Kuwawezesha vijana kujiajiri na kupunguza upungufu wa ajira nchini.

## 6.0 FAIDA ZA MRADI.

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024,*** mradi huu umetuwezesha sisi vijana 16 kupata ajira na kuajiri vijana saba 7 kutokana na faida tuliyopata kwenye mradi, vijana hawa wameajiriwa kwenye shughuli za ufugaji, mgahawa, usafirishaji pamoja na uchomeleaji.
Mradi huu umesaidia kubadili hali za maisha ya wanakikundi mmoja mmoja, Kikundi pia kinachangia kwenye pato la Taifa kwani wanakikundi wanalipa kodi mbalimbali mfano LATRA.

## 5.0 HITIMISHO.

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2024,*** tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi imara uliowezesha kupatikana kwa mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu na hatimae kujikwamua kiuchumi na kujiajiri wenyewe ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025 **Ibara ya 121(a)**

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa***, tunakuomba sasa utembelee na ukague mradi wa kikundi cha vijana cha Gombe.

***" Tunza mazingira na shiriki uchaguzi wa serikali za mitaa kwa ujenzi wa Taifa endelevu" Mwenge wa Uhuru Hoyeeeeeeeeeeeeeeeee***

DAVID YUSUPH KYANDO
**MHASIBU WA KIKUNDI CHA GOMBE**
**KATA YA BONDE LA SONGWE**

# TAARIFA YA MRADI WA UJENZI WA VYUMBA VINNE VYA MADARASA NA MATUNDU MANNE YA VYOO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SONGWE, KWA KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU NDG. GODFREY ELIAKIMU MNZAVA LEO TAREHE 31.08.2024





***Mwonekano wa Mradi wa Madarasa 4 na Matundu 4 ya vyoo shule ya Sekondari Songwe katika picha***

## 1.0 UTANGULIZI

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024,*** Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kuhakikisha inaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia imetekeleza ilani ya uchaguzi **Ibara ya 80(a)** kwa kutoa fedha za ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu manne ya vyoo yaliyojengwa katika shule ya Sekondari Songwe kwa kutumia fedha ya Serikali kuu, nguvu za wananchi, Mapato ya ndani na wadau wengine wa Maendeleo. Ujenzi wa shule hii ulianza rasmi tarehe 01/11/2023 kwa nguvu za wananchi na fedha zilipokelewa tarehe 2/02/2024 kutoka serikali kuu kwa ajili ya uendelezaji wa Mradi. Madarasa haya yatatumiwa na wanafunzi tarajiwa wa kidato cha Tano na Sita.

## 2.0 GHARAMA ZA MRADI

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024,*** Mradi wa ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na matundu manne ya vyoo hadi kukamilika umetumia **Tzs 114,477,200.00** ambazo zimekamilisha Ujenzi wa Vyumba 4 vya madarasa na matundu 4 ya vyoo. Kwa mchanganuo ufuatao;

| NA. | CHANZO CHA FEDHA | KIASI KILICHOTOLEWA | KIASI KILICHOTUMIKA | BAKAA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Michango ya nguvu za wananchi* (harambee na fursa zilizothamanishwa) | 1,857,600.00 | 1,857,600.00 | - |
| 2. | Serikali kuu | 100,000,000.00 | 100,000,000.00 | - |
| 3. | Mbeya Cement trip 7 za Mawe | 3,457,600.00 | 3,457,600.00 | - |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | Michango ya Mwenge | 5,000,000.00 | 5,000,000.00 | |
| 5 | Mchango wa Halmashauri | 4,162,000.00 | 4,162,000.00 | - |
| | **Jumla** | **114,477,200.00** | **114,477,200.00** | **-** |

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MRADI

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024,*** Mradi huu wa majengo ya madarasa manne (4) na matundu manne (4) ya vyoo pamoja na utengenezaji wa Madawati mia moja na sitini (160). umekamilika kwa asilimia 100 tayari kwa kuanza kutumika. Aidha ujenzi umezingatia miundombinu yote ya walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum utaratibu wa manunuzi uliotumika ni **"Force account''.** Aidha, ujenzi wa mradi huu umezingatia viwango vya ubora wa matofali, nondo pamoja na zege.

## 4.0 MANUFAA YA MRADI

***Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024,*** Mradi huu umelenga kuongeza nafasi za wanafunzi wa kitanzania kuchaguliwa kujiunga na Elimu ya Kidato cha Tano na Sita. Hivyo, kupitia mradi huu wanafunzi watakaochaguliwa watapata mazingira bora ya kujifunzia na kupata elimu iliyo bora.

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024,*** Katika kulinda na kuhifadhi mazingira, katika mradi huu tumefanikiwa kupanda jumla ya miti 2300. Tunaendelea kuungana na Serikali katika kuhamasisha uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

## ***5.0*** HITIMISHO

***Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024,*** Naomba kutumia nafasi hii kuishukuru Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia shuleni.

Tunaunga mkono kaulimbiu ya Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka huu isemayo.

***"TUNZA MAZINGIRA NA SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA KWA UJENZI WA TAIFA ENDELEVU" Mwenge wa Uhuru Hoyeeeeeeeeeeeeeeee***

ALIKO T. MBUBA

**KNY: MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA**

TAARIFA YA KONGAMANO LA VIJANA **KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA NDG. GODFREY ELIAKIMU MNZAVA LEO TAREHE 31.08.2024**

## 1.0 UTANGULIZI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024***, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imeandaa kongamano la vijana wapatao 800 wa kiume na wa kike kutoka kata zote 28, Wilayani Mbeya.

## 2.0 LENGO, LENGO LA KONGAMANO

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024***, Lengo la kongamano hili ni kuwapa fursa vijana kujadili,

- Fursa za kiuchumi zilizopo wilayani Mbeya na namna ya kuzitumia
- Kuwawezesha na kuwajenga vijana kuwa wazalendo na waadilifu katika Taifa
- Kuwapa vijana stadi mbalimbali za maisha ili kuwafanya wawe vijana wenye kujitambua zaidi na kuchangia katika ustawi na maendeleo ya jamii
- Kuwajengea vijana stadi za uongozi ili waweze kushiriki vema katika masuala mbalimbali ya uongozi katika jamii
- Ushiriki wa vijana katika uchaguzi wa serikali za Mitaa 2024 (haki na wajibu wa kijana)

## 3.0 UWASILISHAJI WA MADA NA SHUGHULI SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024;***
Katika kongamano hili mada mbalimbali za uzalishaji mali na uongozi zimewasilishwa pamoja na Maonyesho ya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kwa vijana ambapo kikundi cha vijana cha MBEKIWA kimeonyesha shughuli zao za uzalishaji mali na mwisho tumeweka Maazimio ya kongamano kwa mwaka 2024.
Wafuatao wamefanikiwa kutoa mada katika kongamano hili

- Mhe. Mwalingo Kisemba – Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya Mbeya aliwasilisha mada ya Uzalendo na Kujitolea

- Dr. Balongo kutoka chuo kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya amewasilisha mada ya fursa katika mnyororo wa kilimo biashara kwa vijana wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya

- Bw. Julias Mlwafu kutoka UTT aliwasilisha mada ya fursa za Uwekezaji kwa vijana kupitia UTT Amis
- Bwana Alfa Makaye kutoka TCRA aliwasilisha mada ya Faida na Hasara za mitandao ya Kidigitali kwa vijana
- Dr. Beatrice Mwandete kutoka Hospitali ya kanda ya rufaa ya Mbeya aliwasilisha mada ya afya ya akili na Vijana (Msongo wa Mawazo na matumizi ya Dawa za Kulevya
- Bi. Irene Kasonga wanasheria wa Halmashauri aliwasilisha mada ya haki na wajibu wa vijana katika uchaguzi
- Mwl Mwandele Kutoka chuo cha maendeleo ya wananchi Nzovwe kilichopo bonde la songwe aliwasilisha mada ya ujasiriamali na Vijana
- Bi. Paskalina Diu Meneja Mahuiano taasisi za Serikali CRDB aliwasilisha mada ya umuhimu wa Kuweka akiba na fursa za Mikopo (Imbeju)

## 4.0 SHUKRANI

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024;***

Kipekee tunatoa shukrani za dhati kwa mheshimiwa DKT. Samia Suluhu Hassan Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuunganisha vijana na fursa mbalimbali ikiwemo mikopo ya 10% katika halmashauri zote nchini.

***Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa wa Mwaka 2024;*** tunaomba sasa utufungie kongamano letu la vijana,

Sisi ijana wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya tunaunga mkono kaulimbiu ya Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2024 isemayo.

***"TUNZA MAZINGIRA NA SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA KWA UJENZI WA TAIFA ENDELEVU" Mwenge wa Uhuru Hoyeeeeeeeeeeeeeeee***

HADIJA ATHUMANI RAMADHANI
**KNY: MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBEYA**